THE REPUBLIC OF UGANDA

Ministry of Education and Sports

# HOME-STUDY LEARNING

SENIOR 3

## KISWAHILI

August 2020

NCDC
NATIONAL CURRICULUM DEVELOPMENT CENTRE

UGANDA NATIONAL EXAMINATIONS BOARD

NCDC
NATIONAL CURRICULUM
DEVELOPMENT CENTRE

Published 2020

This material has been developed as a home-study intervention for schools during the lockdown caused by the COVID-19 pandemic to support continuity of learning.

Therefore, this material is restricted from being reproduced for any commercial gains.

National Curriculum Development Centre
P.O. Box 7002,
Kampala- Uganda
www.ncdc.go.ug

**FOREWORD**


Following the outbreak of the COVID-19 pandemic, government of Uganda closed all schools and other educational institutions to minimize the spread of the coronavirus. This has affected more than 36,314 primary schools, 3129 secondary schools, 430,778 teachers and 12,777,390 learners.

The COVID-19 outbreak and subsequent closure of all has had drastically impacted on learning especially curriculum coverage, loss of interest in education and learner readiness in case schools open. This could result in massive rates of learner dropouts due to unwanted pregnancies and lack of school fees among others.

To mitigate the impact of the pandemic on the education system in Uganda, the Ministry of Education and Sports (MoES) constituted a Sector Response Taskforce (SRT) to strengthen the sector's preparedness and response measures. The SRT and National Curriculum Development Centre developed print home-study materials, radio and television scripts for some selected subjects for all learners from Pre-Primary to Advanced Level. The materials will enhance continued learning and learning for progression during this period of the lockdown, and will still be relevant when schools resume.

The materials focused on critical competences in all subjects in the curricula to enable the learners to achieve without the teachers' guidance. Therefore effort should be made for all learners to access and use these materials during the lockdown. Similarly, teachers are advised to get these materials in order to plan appropriately for further learning when schools resume, while parents/guardians need to ensure that their children access copies of these materials and use them appropriately.

I recognise the effort of National Curriculum Development Centre in responding to this emergency through appropriate guidance and the timely development of these home study materials. I recommend them for use by all learners during the lockdown.



**Alex Kakooza**
Permanent Secretary
Ministry of Education and Sports

## ACKNOWLEDGEMENTS

National Curriculum Development Centre (NCDC) would like to express its appreciation to all those who worked tirelessly towards the production of home–study materials for Pre-Primary, Primary and Secondary Levels of Education during the COVID-19 lockdown in Uganda.

The Centre appreciates the contribution from all those who guided the development of these materials to make sure they are of quality; Development partners - SESIL, Save the Children and UNICEF; all the Panel members of the various subjects; sister institutions - UNEB and DES for their valuable contributions.

NCDC takes the responsibility for any shortcomings that might be identified in this publication and welcomes suggestions for improvement. The comments and suggestions may be communicated to NCDC through P.O. Box 7002 Kampala or email admin@ncdc.go.ug or by visiting our website at http://ncdc.go.ug/node/13.

**Grace K. Baguma**
Director,
National Curriculum Development Centre

## ABOUT THIS BOOKLET

Dear learner, you are welcome to this home-study package. This content focuses on critical competences in the syllabus.

The content is organised into lesson units. Each unit has lesson activities, summary notes and assessment activities. Some lessons have projects that you need to carry out at home during this period. You are free to use other reference materials to get more information for specific topics.

Seek guidance from people at home who are knowledgeable to clarify in case of a challenge. The knowledge you can acquire from this content can be supplemented with other learning options that may be offered on radio, television, newspaper learning programmes. More learning materials can also be accessed by visiting our website at www.ncdc.go.ug or ncdc-go-ug.digital/. You can access the website using an internet enabled computer or mobile phone.

We encourage you to present your work to your class teacher when schools resume so that your teacher is able to know what you learned during the time you have been away from school. This will form part of your assessment. Your teacher will also assess the assignments you will have done and do corrections where you might not have done it right.

The content has been developed with full awareness of the home learning environment without direct supervision of the teacher. The methods, examples and activities used in the materials have been carefully selected to facilitate continuity of learning.

You are therefore in charge of your own learning. You need to give yourself favourable time for learning. This material can as well be used beyond the home-study situation. Keep it for reference anytime.

Develop your learning timetable to ca ter for continuity of learning and other responsibilities given to you at home.

**Enjoy learning**

KIDATO CHA TATU

MUHULA WA KWANZA

## Mada Kuu 1: VIVUMISHI

### Somo 1:

Vivumishi ni maneno ambayo hutoa habari zaidi kuhusu nomino.

**Malengo**: Baada ya kujifunza somo hili:

-Utaweza kutambua vivumishi vya asili ya kibantu na vile vya asili ya kigeni.

**Unahitaji vifaa kama**: Muda, daftari, kalamu, nakala ya mwanafunzi.

**Utangulizi:** Je, unajua kuwa kivumishi ni kipashio ambacho hutoa maelezo zaidi juu ya nomino?

Katika somo hili utajifunza kuhusu vivumishi vya asili ya kibantu na kigeni.

**Maagizo:** Tafuta pahali mwafaka kusoma makala haya, utafanya mazoezi na shughuli zote zilizomo. Kumbuka kuwa baadhi ya shughuli zinaweza kuchukua muda mrefu. Soma maagizo kwa makini kabla ya kufanya zoezi /shughuli husika.

**Shughuli 1**

Soma mifano ya sentensi yenye vivumishi kwa umoja na wingi (Ngeli ya A-Wa)

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Mtoto **mwema.** | 1.Watoto **wema** |
| 2. Msichana **mzuri.** | 2.Wasichana **wazuri.** |
| 3. Msichana **mchafu** | 3. wasichana **wachafu** |
| 4. Mwalimu **mrefu** | 4.Walimu **warefu** |
| 5. Mwanafunzi **mdogo** | 5.Wanafunzi **wadogo** |

**Shughuli 2**

Tunga sentensi zako mwenyewe tano katika ngeli ya A-Wa kwa kutumia vivumishi

Kwa mfano: 1. Mvulana mfupi (umoja)

-Wavulana wafupi (wingi).

Soma mifano ya sentensi zenye vivumishi vya asili ya kigeni

| **Umoja** | **wingi** |
|---|---|
| 1. Mpishi **safi** | 1.Wapishi safi |
| 2. Mtoto **malidadi** | 2.Watoto malidadi |
| 3. Msichana mmoja | 3. Wasichana wawili |
| 4. Mzazi mchangamfu | 4.Wazazi wachangamfu. |
| 5. Mwimbaji **hodari** | 5.Waimbaji hodari |

*****Utatambua kwamba vivumishi vya asili ya kigeni havizingatii viwakilishi vya nomino husika**

**Shughuli 3**

i) Tunga sentensi tano kwa kutumia vivumishi vya kigeni katika hali ya umoja

ii) Geuza sentensi hizo za vivumishi vya kigeni katika hali ya wingi.

**Zingatia**

Vivumishi mbalimbali ambavyo baadhi ya mifano yake imegawanyika katika aina kuu zifuatazo:

(a) Vivumishi vya sifa.

(b) Vivumishi vya idadi

(ch) Vivumishi viulizi

(d) Vivumishi vya pekee

## Somo 2: Vivumishi vya sifa.

**Malengo**: Baada ya kujifunza somo hili:

-Utaweza kutambua vivumishi vya sifa katika ngeli ya A- Wa (umoja na wingi).

**Unahitaji vifaa kama**: Muda, daftari, kalamu, nakala ya mwanafunzi.

**Utangulizi:** Je, unajua kuwa vivumishi vya sifa ni vivumishi vinavyotaja tabia au vitu vilivivyo au vinavyooenkana?

Katika somo hili utajifunza kuhusu vivumishi vya sifa.

**Maagizo:** Tafuta pahali mwafaka kusoma makala haya, utafanya mazoezi na shughuli zote zillimo. Kumbuka kuwa baadhi ya shughuli zinaweza kuchukua muda mrefu. Soma maagizo kwa makini kabla ya kufanya zoezi /shughuli husika.

### (a) Vivumishi vya sifa

**V**ivumishi vya sifa ni vivumishi vinavyotaja tabia au vitu vilivivyo au vinavyooenkana.

**Kwa mfano;**

-ema, -pevu,-nyamavu, -baya -refu-kamili-changamfu, -ovu

-eusi - kubwa-pumbavu, -nyenyekevu, -danganyifu, zuri-chafu - rahisi

Mifano ya sentensi katika ngeli ya A-wa

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Mkulima **mbaya** | 1. Wakulima **wabaya** |
| 2. Mfalme **mkubwa.** | 2. Wafalme **wakubwa** |

**Shughuli: 4**

Tunga sentensi tano katika ngeli ya A-Wa huku ukitumia vivumishi vya sifa

**Somo 3: Vivumishi vya idadi.**

**Malengo**: Baada ya kujifunza somo hili:

-Utaweza kutambua vivumishi vya idadi katika ngeli ya A- Wa (umoja na wingi).

**Unahitaji vifaa kama**: Muda, daftari, kalamu, nakala ya mwanafunzi.

**Utangulizi:** Je, unajua kuwa vivumishi vya idadi ni vivumishi vinavyoonyesha jumla au hesabu ya vitu.

Katika somo hili utajifunza kuhusu vivumishi vya idadi.

**Maagizo:** Tafuta pahali mwafaka kusoma makala haya, utafanya mazoezi na shughuli zote zillimo. Kumbuka kuwa baadhi ya shughuli zinaweza kuchukua muda mrefu. Soma maagizo kwa makini kabla ya kufanya zoezi /shughuli husika.

**(b) Vivumishi vya Idadi**

Vivumishi vya idadi ni vivumishi vinavyoonyesha jumla au hesabu ya vitu. Kwa mfano

-chache -ingi lukuki maridhawa pungufu

Haba kidogo

Vivumishi vya idadi (hesabu) kwa mfano:

moja , saba, kumi, mia moja, elfu

Elfu tano laki moja milioni kumi bilioni

Mifano ya Sentensi zenye vivumishi vya idadi katika ngeli ya A-Wa

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Msichana maridhawa | 1.Wasichana maridhawa. |
| 2. Mwizi mmoja | 2. Wezi kumi |

3. Mfanyakazi mmoja — 3. Wafanyakazi wengi

4. Mtu mpungufu — 4.Watu wapungufu

5. Mwanamke mmoja — 5.Wanawake wachache

**Shughuli 5**

Tunga sentensi tano katika ngeli ya A-Wa huku ukitumia vivumishi vya Idadi.

## Somo 4

## Vivumishi viulizi.

**Malengo**: Baada ya kujifunza somo hili:
-Utaweza kutambua vivumishi viulizi katika ngeli ya A- Wa (umoja na wingi).

**Unahitaji vifaa kama**: Muda, daftari, kalamu, nakala ya mwanafunzi.

**Utangulizi:** Je, unajua kuwa vivumishi viulizi ni vivumishi vinavyouliza maswali kuhusiana na nomino.

Katika somo hili utajifunza kuhusu vivumishi viulizi.

**Maagizo:** Tafuta pahali mwafaka kusoma makala haya, utafanya mazoezi na shughuli zote zillimo. Kumbuka kuwa baadhi ya shughuli zinaweza kuchukua muda mrefu. Soma maagizo kwa makini kabla ya kufanya zoezi /shughuli husika.

**(ch) Vivumishi viulizi**

Vivumishi viulizi ni vivumishi vinavyouliza maswali kuhusiana na nomino. Kwa mfano

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Gani? | Wapi? | Lini? | -pi? | Ngapi? |
| Je? | Nini? | Nani? | Mbona? | Kwa nini? |

Mifano ya sentensi zenye vivumishi viulizi katika ngeli ya A- Wa

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Ni mtoto gani aliyesoma? | 1.Ni watoto wangapi waliosoma? |
| 2. Mzee anaenda wapi? | 2.Wazeee wanaenda wapi? |
| 3. Mkristo anaomba Mungu lini? | 3.Wakristo wanaomba Mungu lini? |
| 4. Mbona mwanamume amechelewa? | 4.Mbona wanaume wamechelewa? |
| 5. Kwa nini mwalimu alikupiga? | 5. Kwa nini walimu waliwapiga? |

**Shughuli 6**

Tunga sentensi tano katika ngeli ya A-Wa huku ukitumia vivumishi viulizi.

**Somo la 5**

**(d) Vivumishi vya pekee**

**Malengo**:  Baada ya kujifunza somo hili:

-Utaweza kutambua vivumishi vya pekee katika ngeli ya A- Wa (umoja na wingi).

**Unahitaji vifaa kama**: Muda, daftari, kalamu, nakala ya mwanafunzi.

**Utangulizi:** Je, unajua kuwa vivumishi vya pekee ni maumbo?

Katika somo hili utajifunza kuhusu vivumishi vya pekee.

**Maagizo:** Tafuta pahali mwafaka kusoma makala haya, utafanya mazoezi na shughuli zote zillimo. Kumbuka kuwa baadhi ya shughuli zinaweza kuchukua muda mrefu. Soma maagizo kwa makini kabla ya kufanya zoezi /shughuli husika.

Vivumishi vya pekee ni maumbo: Kwa mfano:

- -enye
- -enyewe
- -ote
- -o-ote
- - ingine

(i) **-enye**: Huonyesha nomino yenye kumiliki kitu fulani. Kwa mfano

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| 1. Mtoto mwenye kitabu amekuja. | 1. Watoto wenye vitabu wamekuja. |
| 2.Alisema hawezi kuvaa kiatu chenye tundu. | 2.Walisema hawawezi kuvaa viatu venye matundu |

**Shughuli 1:6**

Tunga sentensi tano katika ngeli ya A-Wa huku ukitumia vivumishi vya pekee (- enye) katika hali ya umoja na wingi.

(ii) **- enyewe**: Kivumishi "enyewe" hutumika kusisitiza nomino fulani. Kwa mfano

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| 1. Mwizi mwenyewe ametoroka. | 1.Wezi wenyewe wametoroka |
| 2. Mtoto mwenyewe ni mchafu. | 2.watoto wenyewe ni wachafu. |

**Shughuli 7**

Tunga sentensi tano katika ngeli ya A-Wa huku ukitumia vivumishi vya pekee (-enyewe) katika hali ya umoja na wingi.

(iii) **- ote:** Huonyesha ujumla wa kitu au vitu. Kwa mfano

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Amekula Mbuzi wote | 1.Wamekula Mbuzi wote |
| 2. Ng'ombe wote ni mweusi | 2. Ng'ombe wote ni weusi |

**Shughuli 8**

Tunga sentensi tano katika ngeli ya A-Wa huku ukitumia vivumishi vya pekee (- ote) katika hali ya umoja na wingi.

(iv) **-o-ote:** Kina maana ya "kila" bila kubagua . kwa mfano

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Mtu yeyote anakaribishwa. | 1.Watu wowote wanakaribishwa. |
| 2. Mgeni yeyote atakula nyama ya kuku. | 2. Wageni wowote watakula nyama ya kuku. |

**Shughuli 9**

Tunga sentensi tano katika ngeli ya A-Wa huku ukitumia vivumishi vya pekee (- o-ote) katika hali ya umoja na wingi.

(v) - **Ingine**: Huonyesha "tofauti "na au "zaidi ya" kitu fulani.

**Kwa mfano:**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Msichana mwingine anapendeza | 1.Wasichana wengine wanapendeza. |
| 2. Mgeni mwingine amefika | 2.Wageni wengine wamefika. |

**Shughuli 10**

Tunga sentensi tano katika ngeli ya A-Wa huku ukitumia vivumishi vya pekee (- ingine) katika hali ya umoja na wingi.

## Zoezi 1:1 Kujaza jedwali

| Nomino | -enye | -enyewe | -o-ote | -ote | -Ingine |
|---|---|---|---|---|---|
| Mzee | **mw**enye | ............ | ........... | ......... | .......,  |
| Wazee | **w**enye | ........... | ............ | ......... | ........ |
| Jibu | **l**enye | .......... | ........... | ......... | ......... |
| Kizazi | **ch**enye | .......... | .......... | ......... | ........ |
| Jiko | **l**enye | ........... | ......... | ......... | ....... |
| Mahali | **P**enye<br>**Kw**enye<br>**mw**enye | ............<br>...........<br>............ | ............<br>...........<br>............ | ............<br>...........<br>............ | ............<br>...........<br>............ |
| Uzi | .......... | ............ | ......... | ......... | ........ |
| Kucheka | .......... | ........... | ......... | ......... | ........ |

## Muhtasari wa mada

Katika mada hii, wanafunzi wamejifunza kuhusu:

- Maana ya vivumishi
- Vivumishi vya sifa
- Vivumishi vya idadi
- Vivumishi viulizi
- Vivumishi vya pekee

## Mada Kuu 2: Vivumishi Virejeshi

## Somo la kwanza

Virejeshi ni viwakilishi ambavyo vina uamilifu wa kukirejea kile kinachowakilishwa. Vivumishi virejeshi ni vya aina mbili:

**Malengo**: Baada ya kujifunza somo hili utaweza:

(i) kutaja virejeshi ( amba- ,na " O rejeshi")

(ii) kutunga sentensi akitumia virejeshi (amba na "O-rejeshi") katika hali ya umoja na wingi

**Utahitaji vifaa kama:** Muda, daftari,kalamu ,kitabu cha Kiswahili.

**Utangulizi:**

Katika somo hili utajifunza kutaja virejeshi – (amba na "O") rejeshi na kuvitumia kutunga sentensi katika hali ya umoja na wingi.

**Maagizo**: Tafuta pahali mwafaka kusoma makala haya. Utafanya mazoezi na shughuli zote zilizomo. Kumbuka kuwa baadhi ya shughuli zinazoweza kuchukua muda mrefu. Soma maagizo kwa makini kabla ya kufanya zoezi/ shughuli husika.

**Vivumishi virejeshi**: Virejeshi ni viwakilishi ambavyo vina uamilifu wa kukirejea kile kinachowakilishwa.

**(a) Amba**

Soma mifano ya sentensi zifuatazo;

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| 1. Mwalimu ambaye anafundisha ni mzungu. | 1. Walimu ambao wanafundisha ni wazungu. |
| 2.Mvuvi ambaye anavua ni mrefu. | 2. Wavuvi ambao wanavua ni warefu. |
| 3. Mlevi ambaye anapiga kelele ni mwanamke | 3. Walevi ambao wanapiga kelele ni wanawake |
| 4.Mtangazaji ambaye anaongea ni msichana. | 4. Watangazaji ambao wanaongea ni wasichana |
| 5. Mbunge ambaye anaongea ni mdanganyifu | 5. Wabunge ambao wanaongea ni wadanganyifu |

**Shughuli 1**

Tunga sentensi tano katika ngeli ya **A-Wa** huku ukitumia kivumishi kirejeshi (amba) katika hali ya umoja na wingi.

**Somo 2: "O" rejeshi (kuondoa amba)**

**Malengo**: Baada ya kujifunza somo hili utaweza:

(i) kutaja na kutambua matumizi ya " O-rejeshi"

(iii) kutunga sentensi akitumia kirejeshi ("O") katika hali ya umoja na wingi

**Utahitaji vifaa kama:** Muda, daftari, kalamu, kitabu cha Kiswahili.

**Utangulizi:** Je, unajua kuwa kirejeshi ni kiwakilishi ambacho kina uamilifu wa kukirejea kile kinachowakilishwa? Katika somo hili utajifunza kutaja virejeshi – ("O") rejeshi na kuvitumia kutunga sentensi katika hali ya umoja na wingi.

**Maagizo**: Tafuta pahali mwafaka kusoma makala haya. Utafanya mazoezi na shughuli zote zilizomo. Kumbuka kuwa baadhi ya shughuli zinazoweza kuchukua muda mrefu.

Soma maagizo kwa makini kabla ya kufanya zoezi/ shughuli husika.

Soma sentensi zinazoonyesha matumizi ya “O” -rejeshi

**Kwa mfano**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| 1. Mwalimu anayefundisha ni mzungu. | 1. Walimu wanaofundisha ni wazungu. |
| 2.Mvuvi anayevua ni mrefu. | 2. Wavuvi wanaovua ni warefu. |
| 3. Mlevi anayepiga kelele ni mwanamke | 3. Walevi wanaopiga kelele ni wanawake |
| 4.Mtangazaji anayeongea ni msichana. | 4. Watangazaji wanaoongea ni wasichana |
| 5. Mbunge anayeongea ni mdanganyifu | 5. Wabunge wanaoongea ni wadanganyifu |

**Shughuli 2**

Tunga sentensi tano katika ngeli ya A-Wa huku ukitumia kivumishi kirejeshi (“o”) katika hali ya umoja na wingi.

**Zoezi 2: 1**

1. Jaza jedwali hili hapa chini kwa kutumia kiresheshi amba-.

| | Ngeli | Mofu | Mifano |
|---|---|---|---|
| 1. | A<br>Wa | Ye<br>o | Mtu ………….;.<br>Watu …………… |
| 2. | U<br>I | O<br>Yo | Mti……………..<br>Miti…………….. |
| 3. | Li<br>Ya | Lo<br>yo | Jicho…………….<br>Macho………….. |
| 4. | Ki<br>Vi | Cho<br>Vyo | Kiti……………..<br>Viti……………… |
| 5. | I<br>Zi | Yo<br>Zo | Nguo…………….<br>Nguo……………. |
| 6. | U | O | Uvuvi………….. |
| 7. | U<br>Ya | O<br>Yo | Ugonjwa ………..<br>Magonjwa………. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 8. | U<br>Zi | O<br>Zo | Ufa……………..<br>Nyufa………….. |
| 9. | Ku | Ko | Kuimba………… |
| 10. | Mahali | Po<br>Ko<br>Mo | Mahali…………..<br>Mahali………….<br>Mahali………….. |
| 11. | Ya | Yo | Maji……………... |
| 12. | I- I | Yo | Chai…………….. |

2. Andika tena sentensi hizi kwa kutumia "O" rejeshi katika sentensi zifuatazo:

(i) Mtu ambaye alikuja jana ni mwizi.

(ii) Mkurugezi ambaye anacheka ni Ssemakula.

(iii) Mkulima ambaye analima ni mwislamu.

(iv) Wanafunzi ambao wanasoma ni wa kidato cha tatu.

(v) Wanasheria ambao wanakuja ni wachina.

## Muhtasari wa mada

Katika mada hii, wanafunzi wamejifunza kuhusu:

- Maana ya virejeshi
- Aina za virejeshi (Amba- na "O rejeshi")
- Utungaji wa sentensi katika hali ya umoja na wingi

## MUHULA WA PILI

## Mada Kuu 1: Ufahamu

### Somo 1:

Ufahamu ni zoezi la kumpa mwanafunzi mbinu za uelewaji na kumjaribu kama anaelewa na alichokisoma.

**Malengo:** Baada ya kujifunza somo hili utaweza:

- Kufasili maana ya vifungu mbalimbali vya maneno,

-Kuorodhesha misamiati uliotumika

- Kujibu maswali.

Utahitaji vifaa kama: Muda, daftari, kalamu,kitabu cha Kiswahili.
**Utangulizi**: Je,unajua kuwa ufahamu ni zoezi la kumpa mwanafunzi mbinu za uelewaji na kumjaribu kama anaelewa na alichokisoma?

## Katika somo hili utajifunza:

- Maswali ya ufahamu

- Jinsi ya kujiandaa kwa ufahamu.

- Umuhimu wa somo la ufahamu.

**Maagizo**: Tafuta pahali mwafaka kusoma makala haya. Utafanya mazoezi na shughuli zote zilizomo. Kumbuka kuwa baadhi ya shughuli zinazoweza kuchukua muda mrefu. Soma maagizo kwa makini kabla ya kufanya zoezi/ shughuli husika.

**Shughuli 1:1**

Soma makala yoyote ya kiswahili na uorodheshe msamiati.

**Ufahamu:** Ufahamu ni somo ambalo humpa mwanafunzi uwezo wa kustawishambinu-zakusoma, kuelewa, kukumbuka, kuhifadhi na kuzingatia yanayosomwa.

Maswali ya ufahamu huwa kama:

**Kuchagua**: Kuchagua ni kujibu swali lililo bora miongoni mwa majibu mengine.

**Kujaliza**: Ni kujaza maneno yaliondolewa ili kukamilisha jibu.

**Kupanga**: Ni kuweka fikira zilizotolewa ili zilete wazo linalonuiwa.

**Kuchagua**: Ni kama kuchagua fikira zilizotolewa ni za ukweli au uongo.

**Kuambatanisha**: Ni kuweka fikira zilizotolewa pamoja na maelezo au sifa zake.

**Kukamilisha**: Ni maelezo pungufu.

**Kujibu swali lililotolewa kwa maneno yako mwenyewe.** Namna hizi za maswali hutegemea taarifa iliyotolewa na ufahamu.

**Somo 2**:

Ufahamu ni zoezi la kumpa mwanafunzi mbinu za uelewaji na kumjaribu kama anaelewa na alichokisoma.

**Malengo:** Baada ya kujifunza somo hili utaweza:

- Kufasili maana ya vifungu mbalimbali vya maneno,

- Kujibu maswali.

**Utahitaji vifaa kama:** Muda, daftari,kalamu, kitabu cha Kiswahili.
**Utangulizi**: Je, unajua kuwa ufahamu ni zoezi la kumpa mwanafunzi mbinu za uelewaji na kumjaribu kama anaelewa na alichokisoma?

Katika somo hili utajifunza:

- Maswali ya ufahamu

- Jinsi ya kujiandaa kwa ufahamu.

**Maagizo**: Tafuta pahali mwafaka kusoma makala haya. Utafanya mazoezi na shughuli zote zilizomo. Kumbuka kuwa baadhi ya shughuli zinazoweza kuchukua muda mrefu. Soma maagizo kwa makini kabla ya kufanya zoezi/ shughuli husika.

**Mambo ya kuzingatia katika kazi ya Ufahamu**:

(i) Unapaswa kusoma kwa makini makala mara ya kwanza huku ukijaribu kukisia ujumbe wake.

(ii) Soma mara ya pili na kukadiria maana ya maneno na istilahi zilizotumiwa.

(iii) Soma maswali yanayoulizwa kwa kuzingatia vifungu vya maneno muhimu na kuvipigia mistari.

(iv) Baada ya kuyasomwa maswali na kuandika hoja muhimu zinazoyajibu kwa kuzingatia sarufi, na uakifishaji bora.

(v) Elewa maagizo ya kila swali.

(vi) Ikiwezekana majibu yawe kwa maneno yako siyo kunakili neno kutoka katika taarifa.

(vii) Majibu yalenge swali.

(viii) Maswaliya matumizi ya lugha na msamiati humtaka mwanafunzi aeleze kama yalivyotumiwa katika habari si kama unavyoelewa.

**Shughuli 2:2**

(i) Soma mambo ya kuzingatia katika kazi ya ufahamu.

(ii) Andika mambo muhimu ya kuzingatia katika kazi ya ufahamu.

**Mfano 1:1**

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

## Mada Kuu 2: Aina za Ndege

Katika nyama zote za ndege nilizowahi kula, sijaona nyama tamu kama ya ndege aitwaye kuku. Wala nyama yake si ngumu. Watu wengine hupenda ndege mwenye minofu mikubwa lakini jambo nisilopenda juu ya minofu hiyo ni kuwa huiva juu juu, lakini ndani huwa mbichi, Hii ndiyo sababu ya mimi kutopenda sana mapaja ya batamzinga.

### Maswali:

(a) Taja aina za ndege katika taarifa.

(b) Mwandishi anapenda kula nyama ya ndege gani?

(c) Kwa nini mwandishi hapendi kula nyama za minofu mikubwa?

(d) Taja ndege wengine watano unaaojua.

**Zoezi 1:1**

*Soma habari hii na kisha ujibu maswali yatakayofuata*

### Ngamia

Ngamia ni mfalme wa Jangwani. Hakuna mnyama anayeweza kuishi jangwani kama Ngamia. Aghlabu yeye huishi zaidi ya miaka arobaini.

Ngamia jike anapokuwa mimba, huzaa mtoto mmoja na kwa muda wa miaka mitatu baada ya kuzaa, Ngamia huendelea kutoa maziwa. Maziwa yake ni matamu kuliko ya Ng`ombe. Ngamia hutoa karibu lita nne kila siku.

Ngamia ana miguu mirefu yenye nguvu sana. Miguu hiyo hukunjika mara nne anapotaka kukaa. Kwato pana ndizo zinazomsaidia asizame katika mchanga wa jangwani. Macho yake yana mifuniko ya kumlinda na vumbi la jangwa. Ngamia anauwezo wa kufunga masikio yake na pua yake ya kujiepusha na maadui ya jangwani.

Mara nyingi, Ngamia hufikia mita tisa kwa urefu. Mgongoni ana nundu ambayo ni mfano wa ghala ya akiba ya chakula. Anaposhikwa na njaa basi yeye hutumia chakula cha kutosha kutoka kwenye nundu yake. Hivyo basi Ngamia huweza kukaa siku kumi bila ya kuhitaji chakula au maji.

Ngamia ni msaidizi mkuu wa watu wa jangwani kwa kubeba mizigo mizito na kwenda mwendo mrefu sana. Ngamia anaweza kubeba mizigo ya kilo mia mbili na kwenda mwendo wa kilomita arobaini kwa muda wa siku tatu mfululizo. Kazi ya kubeba mizigo huianza akiwa na umri wa miaka sita.

Tunafaidika na nyama, maziwa na ngozi ya Ngamia. Tunaweza kutengeneza mikoba, viatu, viriba na vifaa vingine kutoka kwa ngozi yake.

## Maswali

(a) Ngamia huishi wapi?

(b) Ngamia huishi miaka ngapi?

(c) Ngamia hutoa maziwa kwa muda gani baada ya kuzaa?

(d) kwa siku moja, Ngamia hutoa kiasi gani cha maziwa?

(e) Ngamia anawezaje kutozama jangwani?

(f) Nundu ina kazi gani kwa Ngamia?

(g) Ngamia anaweza kukaa siku ngapi bila ya kuhitaji ya chakula?

(h) kwa siku moja, Ngamia anaweza kwenda mwendo wa kilomita gani?

(i) Ngamia hutumiwa sana kwa kazi gani?

(j) toa maana ya maneno haya kama yanavyotumiwa katika taarifa:

(i) Mfalme wa jangwani

(ii) hukunjika

(iii) kwato pana

(iv) nundu

(v) vumbi la jangwa

## Muhtasari wa mada

Katika mada hii, wanafunzi wamejifunza kuhusu:

- Maana ya ufahamu
- Kufasili maana ya vifungu mbalimbali vya maneno,

- Kuorodhesha misamiati ilitumika,
- Kuchambua mbinu za lugha
- Kusoma na kujibu maswali.

## Mada Kuu 2: Uandishi wa Insha

### Somo 1

Insha ni mtungo mwanana wa kisanii wenye ubunifu ambao umeandikwa kwa utaratibu kuhusu jambo fulani.

**Malengo**: Baada ya kujifunza somo hili utaweza:

- Kujifunza hatua na kanuni za utungaji bora wa insha,

-Mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha.

-Uainishaji wa insha (kategoria za insha)

- Sehemu za insha.

**Utahitaji vifaa kama:** Muda, daftari, kalamu, kamusi.

**Utangulizi:** Je, unajua kuwa Insha ni mtungo mwanana wa kisanii wenye ubunifu ambao umeandikwa kwa utaratibu kuhusu jambo fulani?

Katika somo hili utajifunza:

-Sehemu za insha

- Hatua na kanuni za utungaji bora.

- Uainishaji wa Insha.

**Maagizo**: Tafuta pahali mwafaka kusoma makala haya. Utafanya mazoezi na shughuli zote zilizomo. Kumbuka kuwa baadhi ya shughuli zinazoweza kuchukua muda mrefu. Soma maagizo kwa makini kabla ya kufanya zoezi/ shughuli husika.

**Shughuli 3:1**

(i) Soma kazi ya utungaji wa insha.

(ii) Ataje sehemu za insha.

Insha ni mtungo mwanana ambao hugawanywa katika sehemu tatu kuu yaani:

-**Utangulizi**: mwanzo wa insha.

- **Maelezo**: Hii ndiyo sehemu kubwa (maelezo mengi sana)

-**Mwisho**- Hapa ndipo kikomo cha insha.

**Maagizo**: Tafuta pahali mwafaka kusoma makala haya. Utafanya mazoezi na shughuli zote zilizomo. Kumbuka kuwa baadhi ya shughuli zinazoweza kuchukua muda mrefu. Soma maagizo kwa makini kabla ya kufanya zoezi/ shughuli husika.

## Mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha.

1. Kichwa au Anwani: Insha: Insha sharti iwe na kichwa au Anwani inayofaa.

2. Vidokezi au Mpango: Huu ni mpango wa insha kuanzia utangulizi hadi hitimisho wa insha.

3. Utangulizi: Hii ni aya ya kwanza kufafanua mada inayoshughulikiwa. Utangulizi usiwe mrefu sana.

4. Maudhui au Ujumbe: Maudhui au ujumbe sharti hujitokeze katika insha.

5. Sarufi: Maudhui huelezwa kwa lugha sanifu.

6. Mtiririko: Aonyeshe kuwa insha yake ina mtiririko katika mpangilio wa vitushi kuanzia mwanzo hadi mwisho.

7. Mpango wa Lugha: Tumia methali, misemo au nahau kuipamba kazi yako.

8. Hitimisho: Huu ni mhutasari wa insha yako. Lazima uwe na mvuto ule ule ulioanzisha insha na uwe mfupi.

**Shughuli 4:1**

(iii) Soma kazi ya utungaji wa insha.

(iv) Ataje sehemu za insha.

**Somo 2**:

Insha ni mtungo mwanana wa kisanii wenye ubunifu ambao umeandikwa kwa utaratibu kuhusu jambo fulani.

**Malengo**: Baada ya kujifunza somo hili utaweza:

- Kujifunza hatua na kanuni za utungaji bora wa insha,

-Mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha.

-Uainishaji wa insha (kategoria za insha)

- Sehemu za insha.

**Utahitaji vifaa kama:** Muda, daftari ,kalamu,kamusi.

**Utangulizi:** Je, unajua kuwa Insha ni mtungo mwanana wa kisanii wenye ubunifu ambao umeandikwa kwa utaratibu kuhusu jambo fulani?

Katika somo hili utajifunza:

-Sehemu za insha

- Hatua na kanuni za utungaji bora.

- Uainishaji wa Insha.

**Maagizo**: Tafuta pahali mwafaka kusoma makala haya. Utafanya mazoezi na shughuli zote zilizomo. Kumbuka kuwa baadhi ya shughuli zinazoweza kuchukua muda mrefu. Soma maagizo kwa makini kabla ya kufanya zoezi/ shughuli husika.

Insha huainishwa katika aina kuu mbili:

(a) Insha za ubunifu au ndefu

(b) Insha za kiuamalifu au fupi

## 1. Insha zakiuamilifu au fupi

Ni maandishi yenye mtindo maalum na hutumika katika mazingira halisi kwa kuzingatia mtindo huo rasmi. Kwa mfano

(i) Barua

(ii) Ripoti

## 1. Insha za barua

Kuna aina mbili za barua yaani Barua rasmi na Barua ya kirafiki

**(a) Barua ya kirafiki**

Barua ya kirafiki ni barua ambayo mtu huandika kwa mwenzake au mtu wa familia yake. Pia ni barua wanazoandika ndugu, jamaa na marafiki ili kujuliana hali au kupashana habari. Barua hii haichukui mtindo wowote maalum wa kuandikwa. Huwa na anuani moja tu: ya mpokeaji.

Barua hii haitumii lugha rasmi na mwandishi anaweza kumrejelea mwandikiwa kwa kutumia jina lake la kwanza. Aidha barua za kirafiki hazihitaji kutiwa saini.

## Mambo muhimu ya kuzingatia:

**(a) Anwani ya mwandishi na tarehe:**

- Huandikwa juu ya upande wa kulia wa karatasi.
- Mtindo wa mshazari au wima hutumiwa.
- Uakifishaji. Kila mstari huanza kwa herufi kubwa na kuwekwa koma (,) mwishoni isipokuwa mstari wa mwisho ambapo nukta au kitone hutumiwa.
- Jina la mji huandikwa kwa herufi kubwa na chini yake huandikwa tarehe.

Tanbihi: Mwandishi asiandike jina katika anwani, bali mwishoni pa barua.

**(b) Maamkizi:** Huandikwa kwa upande wa kushoto na hutegemea uhusiano kati ya mwandishi na anayeandikiwa. Baada ya maamkizi alama ya koma huwekwa kwa mfano: kwa Baba mpendwa, Mamampendwa, dada, ndugu, Kwa mpenzi, nk

**(ch) Mwanzo:** huanza kwa salamu na kujulia hali.

**(d)Maelezo/Ujumbe**: Mwandishi hutaja lengo la kuandika. Hii ndiyo sehemu inayojibu swali katika insha. Kila wazo kuu sharti liwe katika aya yake. Lugha inayotumiwa huwa ya kirafiki.

**(e) Hitimisho**: Maneno ya kirafiki au kidugu hutumiwa. Kwa mfano; Mwanao mpendwa wako wa daima, mpenzi wako,mwanao mtiifu,rafiki yako wa kufa kuzikana nk

**Mfano 1:1**

**Swal**i: Mwandikie mama yako barua ukimwelezea maisha yako shuleni.

Shule ya upili ya Mella Seed,

S.L.P, 630,

Tororo.

20/04/2020

Kwa Mama mpendwa,

Shikamoo Mama? Nyumbani hamjambo? Habari ya Baba? Dada na Ndugu? Natumaini mko salama salimini. Mimi ni mzima na hapa shuleni maisha ni poa ila ni kupambana na masomo. Mama, nimekuwa na ugonjwa wa mafua na homa ya Malaria hivi juzi.

Nimekuandikia barua hii Mama, nikitaka kukwambia kwamba nilifika shuleni vizuri na tumeishafanya mitihani ya mwanzo wa muhula wa tatu. Pia ninataka kukwambia kuwa vitabu nilivyonunua vimemalizika. Ninaomba unitumie pesa za kununua vitabu, kalamu na matumizi hapa shuleni.

Shuleni, maisha ni mazuri yaani tunafundishwa vizuri, tunakula vizuri yaani kila Jumapili tunakula nyama na ndizi. Wali na nanasi tunapewa kila Jumatano. Tumekuwa na michezo yaani soka, netiboli,mpira wa wavu na kikapu. Pia tumekuwa na michezo ya riadha kama vile jukwe, kuruka na bweni langu la Mandela lilishinda na kupewa Mbuzi, muziki na soda.

Ebu, nimalizie hapa ninakuomba uwasalimie wote nyumbani yaani baba, kaka na dada. Mungu awabariki!

Ni mimi mtoto wako akupendaye.

Scovia Abachi

**Zoezi 1:1**

Kaka yako aliondoka nyumbani mwaka jana na kwenda kufanya kazi katika nchi jirani. Tangu aondoke hamjapata kuonana wala kuwasiliana naye. Mwandikie barua ukimjulisha hali za nyumbani za kisasa nchini mwako. Tumia kati ya maneno 100 – 150.

**Somo 3: Ripoti**

Ni taarifa inayoeleza kuhusu jambo, mtu, shughuli au tukio kwa lengo fulani. Huandikwa kwa usemi wa taarifa.

**Malengo**: Baada ya kujifunza somo hili utaweza:

- Kujifunza hatua na kanuni za utungaji bora wa ripoti,

-Mambo ya kuzingatia katika uandishi wa ripoti.

**Utahitaji vifaa kama:** Muda, daftari ,kalamu,kamusi.

**Utangulizi:** Je, unajua kuwa ripoti ni taarifa inayoeleza kuhusu jambo, mtu,shughuli au tukio kwa lengo fulani?

**Maagizo**: Tafuta pahali mwafaka kusoma makala haya. Utafanya mazoezi na shughuli zote zilizomo. Kumbuka kuwa baadhi ya shughuli zinazoweza kuchukua muda mrefu. Soma maagizo kwa makini kabla ya kufanya zoezi/ shughuli husika.

## Ripoti

Ni taarifa inayoeleza kuhusu jambo, mtu, shughuli au tukio kwa lengo fulani. Huandikwa kwa usemi wa taarifa.

### Sehemu muhimu katika insha ya ripoti

1. **Kichwa**: Hutaja mada na tarehe. Huandikwa kwa herufi kubwa na kupigiwa mstari.

2. **Utangulizi**: Hutaja ripoti kwa muhtasari.

3. **Maelezo au mwili**: Huzungumziwa juu ya ujumbe wenyewe.

4. **Mapendekezo**: Hutolewa lengo la kutoa suluhisho.

5. **Hitimisho:** Sehemu hii iwe na jina, sahihi, tarehe na cheo cha aliyeandika.

## Mfano 1:1

**Swali**: Wewe ni ripota wa gazeti la Monitor. Andika taarifa itakayosomwa na kuonyeshwa kwa runinga juu ya moto uliotokea katika soko la Owino jijini Kampala.

### RIPOTI YA MOTO ULIOTOKEA KATIKA SOKO LA OWINO JIJINI KAMPALA TAREHE 24/10/2018.

Ilikuwa Jumamosi tarehe 24/10/2018, moto uliotokea katika soko la Owino jijini Kampala.

Moto ulianza kuwaka saa tatu za usiku baada ya wafanya biashara wa soko hilo kurudi nyumbani. Chanzo cha moto huo kilitokana na moto wa jiko kuchoma waya za umeme. Wapishi wa soko la Owino hawakufunika meko yao vizuri na moto uliachwa ukiwaka. Moto ulianza na kuchoma vyombo vya kupikia kama vile masufuria, sahani na viti vya mbao vya kukalia. Moto ulienea hadi upande wa wafanya biashara wanao uza nguo na bidhaa nyingine. Mwishoni nyumba zikateketekea au kuchomwa na moto sana.

Mapendekezo juu ya moto ni kama ifuatayo: wapishi wawe waangalifu kuhusu kukinga moto, wafanya biashara wazimishe taa na kutoa swichi za umeme kabla ya kurudi nyumbani. Wawe na walinzi au askari ambao wataripoti kwa Polisi ili walete magari na vifaa vya kuzima moto mapema kabla ya nyumba kuteketea.

Ni mimi mwaminifu,

amoit

Isaac Amoit

Ripota wa gazeti la monitor.

**Zoezi 2:1**

Kulitokea ajali ya ajabu uliyoshuhudia karibu na shule yako. Andika ripoti ukiarifu Polisi juu ya ajali hiyo. Tumia maneno kati ya 100- 150

**Somo 4**:

## Insha za ubunifu / ndefu:

**Malengo**: Baada ya kujifunza somo hili utaweza:

- Kujifunza hatua na kanuni za utungaji bora wa insha,

-Mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha za methali.

**Utahitaji vifaa kama:** Muda, daftari ,kalamu,kamusi.

**Utangulizi:** Je, unajua kuwa Insha za methali ni zinzofunza maana na matumizi yake?

**Maagizo**: Tafuta pahali mwafaka kusoma makala haya. Utafanya mazoezi na shughuli zote zilizomo. Kumbuka kuwa baadhi ya shughuli zinazoweza kuchukua muda mrefu. Soma maagizo kwa makini kabla ya kufanya zoezi/ shughuli husika.

## Insha za ubunifu / ndefu

Insha za ubunifu hujitokeza kama:

- Insha za methali
- Insha za mdokezo

(a) Insha za Methali: Huhitaji vidokezo vinavyoweza kufaa katika uandishi wake.

(i) Eleza maana ya methali na muundo wake.

(ii) Eleza matumizi ya methali hiyo katika matukio tofauti ya maisha na funzo linajitokeza.

(iii) Simulia kisa au visa au matukio yanayodhihirisha ukweli wa methali hiyo.

(iv) Waweza ukataja methali zingine zenye maana moja na methali hiyo.

## Mambo ya kuzingatia katika insha ya methali:

- Anwani au kichwa huwa ni methali yenyewe ilitolewa katika swali.
- vidokezo au mpango.
- Utangulizi: katika aya ya kwanza ni vizuri kueleza maana ya ndani na matumizi yake.
- Mwili:hii ni sehemu ya maudhui. hapa ndipo kisa au visa vitasimuliwa katika aya mbalimbali.
- Mawazo: yatiririshwe moja kwa moja katika mafungu ya aya.
- Hitimisho: methali yenyewe itajwe tena au nyingine yenye maana sawa na inayojadiliwa itolewe.
- mwanafunzi anahitajika kufahamu methali nyingi iwezekanavyo.

## Mfano 1:1

**Swali:** msiba wa kujitakia hauna kilio.

## Msiba wa kujitakia hauna kilio

## vidokezo

- maana na matumizi ya methali
- wahusika
- mahali jambo hilo linapotendewa
- kisa kinachohusiana na methali
- hitimisho

Msiba wa kujitakia hauna kilio ina maana ya kuwa mtu kujiingiza katika shida au tatizo kama vile ulevi, uasherati,uvutaji wa sigara hakuna wakumhurumia ila ni kumchekea. methali hii inatumiwa kuwaambia watu ambao walijiingiza katika taabu au shida na mwishoni kulia au kujuta.

katika shule letu la upili la masooli, kulikuwa na mwanafunzi ambaye alijulikana kwa jina la Okello James. okello james ni mvulana mfupi, mweusi titi,mnene na akisoma kidato cha nne.Okello alikuwa mkaidi sana akipiga kelele darasani wakiwemo walimu. alikata masomo sana na kujidanganya kuwa anasoma usiku. alikuwa akikata vipindi vya

masomo ya Hisabati akijificha nyuma ya bweni la wavulana na akidai kuwa mwalimu wa Hisabati anafundisha vibaya na hisabati ngumu sana.

Siku moja, wakati wa alasiri  mwalimu mkuu alikuwa akitembea tembea shuleni akifanya utafiti kuhusu wanafunzi,kwa nini wanafunzi wanakata vipindi vya masomo ya alasiri? Okello ambaye ni kiongozi wa genge la majambazi shuleni. kikundi chao kilikuwa cha wanafunzi watano na wanafunzi shuleni walikiita “watano wabaya”

Wanafunzi hao watano walishikwa na mwalimu mkuu akiwemo Okello. mwalimu mkuu bila kusita alipigia polisi kwa kuwa wanafunzi hao walikuwa wakitumia na kuvuta dawa za kulevya kama vile marijuana,banji na sigara,kutokana na sheria za shule ni kufukuzwa shuleni na kupelekwa jelani. kwa kuwa asiyesikia la mkuu huvunjika guu. mwalimu mkuu aliwapigia wazazi wake Okello. Wazazi wa Okello walikuja haraka na kumkuta Okello katika kituo cha Polisi ameishatiwa mbaroni au kufungwa jelani.

Baada ya wazazi wake Okello kufika kwa Polisi,walikutana na mkuu wa kituo hicho cha Polisi,aliamua kuwa wanafunzi hao wachapwe viboko kumi kila siku kwa siku saba na kufanya kazi ya umma kama kufagia na kusafisha barabara.

Okello alikuwa anatoka katika familia ya kimaskini hakuendelea na masomo na wale wengine wanne, wazazi wao walikuwa matajiri waliwabadlishia shule na kuwapeleka katika mashule mengine. Okello alikuwa na ndoto ya kuwa wakili au mwanasheria kwa kuwa majuto ni mjukuu. Okello sasa anaishi kijijini na ni maskini hohehahe hana mbele wala nyuma. Okello amebaki na kuuliza na kuongea juu ya mashule aliyosomea na wanafunzi aliosoma nao.

Kwa kweli, msiba wa kujitakia hauna kilio kutokana na maisha Okello anayoishi.

Maneno: 405

**Zoezi 1:1**

Mama wa kambo si mama.

**Somo 5:**

**Insha za mdokezo**: Insha ya aina hii huwa ina kianzo ili mwanafunzi aendeleze au kimalizio ili mwanafunzi amalizie insha yake

**Malengo**: Baada ya kujifunza somo hili utaweza:

- Kujifunza hatua na kanuni za utungaji bora wa insha za mdokezo,

-Mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha za mdokezo.

**Utahitaji vifaa kama:** Muda, daftari ,kalamu,kamusi.

**Utangulizi:** Je, unajua kuwa Insha za mdokezo huwa ina kianzo ili mwanafunzi aendeleze au kimalizio ili mwanafunzi amalizie insha yake?

**Maagizo**: Tafuta pahali mwafaka kusoma makala haya. Utafanya mazoezi na shughuli zote zilizomo. Kumbuka kuwa baadhi ya shughuli zinazoweza kuchukua muda mrefu. Soma maagizo kwa makini kabla ya kufanya zoezi/ shughuli husika.

## INSHA ZA MDOKEZO

Insha ya aina hii huwa ina kianzo ili mwanafunzi aendeleze au kimalizio ili mwanafunzi amalizie insha yake. Mwanafunzi ahakikishe kuwa kuna mtiririko kati ya insha yake na kimalizio au kianzo alichopewa.

**Mfano 1:1**

**Swali:** Sauti za umati wenye hasira zilisikika zikisema,"Ua! Mwizi ua! Maliza......." Endelea

## Siku za mwizi ni arobaini

Vidokezo

- Ilikuwa lini?
- Mahali gani palipokuwa na mwizi?
- Kisa cha kumpiga mwizi
- Ni nini kilichotokea baadaye?
- Pendekezo juu ya kisa hicho

Sauti za umati wenye hasira zilisikika zikisema,"Ua! Mwizi ua! Maliza! Choma!... nk

Nilivuta nadhari yangu kwenye upande wa mji wa Mbarara, sauti zilisikika,siamini nilichoshuhudia.

Umati mkubwa ulikuwa umezingira kitu ambacho hakikuonekana vizuri. Baadhi yao walikuwa na makopo ya petroli, wengine mafuta ya taa na wengine walikuwa na mawe na magogo. Ungedhani walikuwa wakikubaliana vita na zimwi la mazimwi.

Mwanzoni nilijawa na woga, kisha nikaona kuwa penye umati mkubwa vile,Yule adui hangeweza kumdhuru yeyote. Nilijikakamua nikasogea ili nishuhudie mwenyewe. Niliiona pandikizi la mtu lililokuwa limepiga magoti na kuinua mikono yake juu. Lilikuwa katika hali ya kuomba msamaha. Tayari mtu yule alikuwa amepigwa kwa inzirani kila sehemu ya mwili wake, zingine zikaacha alama na zingine zikamuumiza na kutoa damu.

Baadhi ya watu walimuuliza maswali ya kijinga kwa mfano" una mikono"? alipojibu aliambiwa kuwa yaelekea kuwa hakuihitaji na basi ingevunjwa. Kando kidogo palikuwa na mwanamke aliyebeba mtoto mgongoni mwake. Kinyume na watu wale wengine, alikuwa ana imani na mtu yule. Aliwasihi wasimtoe roho. Aliwaambia kuwa kipigo alichokuwa amepata kilitosha. Hata hivyo hawakutaka kumsikia.

Nilisongea karibu na bibi yule ili anieleze ni nini kikiendelea. aliniambia kuwa alipokuwa akivuka kukimbilia basi,bwana yule alimyaka mkoba wake na kukimbia nao.alipong'amua alipiga unyende.waliposhuhudia walikimbia na kumshika mwizi huyo.ndipo sasa akaupata mkoba wake na watu wakataka kumfunza tabia mwizi yule.

Aliponihadithia habari ile niliona huzuni na kumuuliza kilichomfanya amhurumie. Aliniambia kuwa kwanza mkoba wake haukuwa na cha maana ila napi za mtoto zilizokuwa zimetumika. Pili, aliona kuwa kuenda mwizi yule akabadhi tabia na kuongoka.

Alipokuwa akisema vile mtu mmoja maalum alimrushia petroli yule na kwa bahati nzuri pakawa hapa kuwa na aliyekuwa na kiberiti nao Polisi wakafika. Walimshika mtu yule na kumwingiza kwenye gari lao na kuenda naye pamoja na mama aliyeibiwa mkoba wake.

Baada ya Polisi kuondoka wakasimulia. Niling'amua kuwa mwizi yule alikuwa akijulikana kuwa hakuwa na kazi maalum na aliwahangaisha wengi ila hakuwa amefumaniwa. Siku hiyo ndiyo aliyotimiza arubaini zake.

Maneno: 456

**Zoezi 1:1**

(i) Tunga insha inayomalizia kwa," .......... Niliamua kuwa kamwe sitawahi kucheza na nguvu za umeme."

Muhtasari wa mada:

- Kujifunza hatua na kanuni za utungaji bora wa insha ,
- Mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha.
- Uainishaji wa insha
- Sehemu za insha

## MUHULA WA TATU

### Mada Kuu 1: Sentensi Za Masharti

**Somo 1**:

Sentensi za Masharti ni zile ambazo hutumia mofu kabla ya mzizi wa kitenzi.
**Malengo:**
Baada ya kujifunza funzo hili,
-Utaweza kutumia mofu hizi kwa kutunga sentensi kwa hali ya kukubali.
- Hali ya kukanusha.
**Utahitaji vifaa kama**: muda, daftari,kalamu , nakala ya mwanafunzi,kamusi
**Utangulizi**: Je, unajua kwamba sentensi za masharti hutumia viwakilishi au mofu tatu?
**Maagizo**: Tafuta pahali mwafaka kusoma makala haya. Utafanya mazoezi na shughuli zote zilizomo. Kumbuka kuwa baadhi ya shughuli zinaweza kuchukua muda mrefu. Soma maagizo kwa makini kabla ya kufanya zoezi /shughuli husika.

**Hali ya ki-**
Kiambishi "Ki" kuonyesha Masharti
*** onyesha kwamba katika hali ya kukanusha, -ki- ya masharti huwa -sipo-

| 1. **Hali ya kukubali** | **Hali ya kukanusha** |
|---|---|
| (a) Watu wakifa huzikwa kaburini | (a) Watu wasipokufa hawazikwi kaburini. |
| (b) Nikisoma kwa bidii nitapita mithani. | (b) Nisiposoma kwa bidii sitapita mitihani |
| (c) Nikipata pesa nitanunua gari. | (ch) Nisipopata sitapatanunua gari |
| (d) Nikilima shambani nitapata mazao mazuri. | (d) Nisipolima shambani sitapata mazao mazuri |
| (e) Tukiamka mapema nitapata gari. | (e) Tusipoamka mapema sitapata gari. |

**Shughuli 1:1**
(i) Kusoma sentensi za hali ya ki masharti hapo juu katika hali ya kukubali na kukanusha.
(ii) Andika sentensi za hali ya ki masharti tano katika hali ya kukubali na kukanusha.

## Somo 2: Hali ya Nge

Viwakilishi hivi huwakilisha masharti. Huonyesha kuwa kitendo fulani hakikutokea. Kutotokea kwake kunasababisha kutokea kwa kitendo kingine ambacho kingetarajiwa kufuata.
Kitendo cha kwanza
**Malengo:** Baada ya kujifunza funzo hili,
-Utaweza kutumia hali ya nge kwa kutunga sentensi kwa hali ya kukubali.
- Hali ya kukanusha.
**Utahitaji vifaa kama**: muda, daftari, kalamu, nakala ya mwanafunzi, kamusi
**Utangulizi**: Je, unajua kwambahuwakilisha masharti.?
**Maagizo**: Tafuta pahali mwafaka kusoma makala haya. Utafanya mazoezi na shughuli zote zilizomo. Kumbuka kuwa baadhi ya shughuli zinaweza kuchukua muda mrefu. Soma maagizo kwa makini kabla ya kufanya zoezi /shughuli husika.

**Hali ya nge,**
Viwakilishi hivi huwakilisha masharti. Huonyesha kuwa kitendo fulani hakikutokea. Kutotokea kwake kunasababisha kutokea kwa kitendo kingine ambacho kingetarajiwa kufuata.
Kitendo cha kwanza kwa mfano
****katika mtindo wa kukanusha, -nge- huwa -singe-**

| **Hali ya kukubali** | **Hali ya kukanusha** |
|---|---|
| 1. Ningesoma kwa bidii, ningejiunga na chuo kikuu. | 1. Nisingesoma kwa bidii nisingejiunga na chuo kikuu. |
| 2.Ningepata pesa ningenunua redio. | 2.Nisingepata pesa nisingenunua redio. |
| 3. Tungefika mapema tungepanda basi. | 3. Tusingefika mapema tusingepanda basi. |
| 4. Angekimbia haraka angepata zawadi. | 4. Asingekimbia haraka |

asingepata zawadi.
5. Mngeungana pamoja mngewashinda. 5. Msingeungana pamoja msingewashinda.

**Shughuli 1:1**

Andika sentensi tano za hali ya nge masharti katika hali ya kukubali na kukanusha.

**Somo 3: Hali ya Ngali/ ngeli**

Viwakilishi hivi huwakilisha masharti. Huonyesha kuwa kitendo fulani hakikutokea. Kutotokea kwake kunasababisha kutokea kwa kitendo kingine ambacho kingetarajiwa kufuata.
Kitendo cha kwanza

**Malengo:** Baada ya kujifunza funzo hili,
-Utaweza kutumia hali ya ngali/ngeli kwa kutunga sentensi kwa hali ya kukubali.
- Hali ya kukanusha.

**Utahitaji vifaa kama**: muda, daftari,kalamu , nakala ya mwanafunzi,kamusi

**Utangulizi**: Je, unajua kwambahuwakilisha masharti.?
**Maagizo**: Tafuta pahali mwafaka kusoma makala haya. Utafanya mazoezi na shughuli zote zilizomo. Kumbuka kuwa baadhi ya shughuli zinaweza kuchukua muda mrefu. Soma maagizo kwa makini kabla ya kufanya zoezi /shughuli husika.

**Hali ya ngali au ngeli**
Viwakilishi hivi huwakilisha masharti. Huonyesha kuwa kitendo fulani hakikutokea. Kutotokea kwake kunasababisha kutokea kwa kitendo kingine ambacho kingetarajiwa kufuata.
Kitendo cha kwanza kwa mfano

## Hali ya kukubali

## Hali ya kukanusha.

1. Ngingalipata pesa ningalinunua gari. 1. Nisingalipata pesa nisingalinunua gari.
2. Tungaliamka mapema tungalipanda basi. 2. Tusingaliamka mapema tusingalipanda basi.
3. Angelipika chakula mapema angelilala. 3. Asingelipika mapema asingelilala.
4. Angefanya mazoezi haraka angerudi nyumbani. 4. Asingelifanya mazoezi haraka asingelirudi nyumbani.
5. Mtoto angelipata chakula mapema angelienda kucheza. 5. Mtoto asingeli pata chakula mapema asingelienda kucheza.

****utagundua kwamba katika hali ya kukanusha –ngali/ngeli huwa –singali/ singeli**

**Shughuli 1:1**

(iii) Kusoma sentensi za hali ya ngali/ngeli masharti hapo juu katika hali ya kukubali na kukanusha.

(iv) Andika sentensi tano za hali ya ngali/ngeli masharti katika hali ya kukubali na kukanusha.

**Zoezi 1:1**

1. Geuza sentensi hizi katika hali ya kukanusha

(a) Ningalipata pesa ningalinunua nyumba.

(b) Ningelipata pesa ningelienda mjini Tororo.

(ch) Angekuja leo ningeenda naye.

(d)Mvua ingelinyesha ningelipanda mahindi.

(a) Mwalimu angalitupa mtihani mapema tungalifaulu.

## Muhtasari wa mada

Katika mada hii, wanafunzi wamejifunza kuhusu:

- Kutunga sentensi kwa hali ya ki masharti
- Kutunga sentensi kwa hali ya nge masharti
- Kutunga sentensi kwa hali ya ngali/ngeli masharti
- Kutunga sentensi za masharti katika hali ya kukubali na kukanusha katika ngeli ya A- Wa.

## Mada Kuu 2: Methali Za Kiswahili

### Somo 1: Methali za kiswahili

Methali ni fungu la maneno ambalo lenye maana fiche. Methali hufunza, hutahadharisha, huonya,hutunza maadili nk

**Malengo:** Baada ya somo hili:

-Utaweza kuchambua maana ya methali.

- Utaweza kuchambua matumizi ya methali.

**Utahitaji vifaa kama**: Daftari, Kalamu,Kamusi ya methali.

**Utangulizi**:

Je, unajua kwamba methali ni fungu la maneno yenye maana fiche.

Uchambuzi wa methali juu ya maana ya juu juu na maana ya ndani. Eleza maana ya methali na umaarufu wake na matumizi ya methali hiyo

**Maagizo**: Tafuta pahali mwafaka kusoma makala haya. Utafanya mazoezi na shughuli zote zilizomo. Kumbuka kuwa baadhi ya shughuli zinaweza kuchukua muda mrefu. Soma maagizo kwa makini kabla ya kufanya zoezi /shughuli husika.

**Umuhimu wa methali**

Umuhimu wa methali ni kama:

- Kujenga ustadi wa lugha (kipawa cha kutafakari)
- Kuonya au kukejeli binadamu
- Kuelimisha watu

- Hutumika kuburudika

**Shughuli 1:1**

(i) Soma methali za Kiswahili hizi
(ii) Andika methali hizi kwa kitabu.

.
Baadhi ya methali ni kama zifuatazo:
1. Baada ya dhiki faraja
(Hutumika kumpa mtu nguvu za kushughulikia akitakacho)
2. Hasira hasara. (Humonya mtu dhidi ya wepesi wake wa kuamua juu ya jambo fulani)
3. Kuishi kwingi ni kuona mengi.
(Uzoefu wa mtu juu wa matakwa ya dunia)
4. Mchovya asali huchovya mara moja.
(Twendelee na shughuli mara kadhaa mpaka tutakapofaulu)
5. Njaa leo ni shibe ya kesho.
(Tuwe tuna akiba ya kesho)
6. Akipenda chongo huita Kengeza.
7. Mama wa kambo si mama.
8. Heri kenda shika kuliko kumi nenda rudi.
9. Kupotea njia ndiko kujua njia.
10. Maji hufuata mkondo.

**Zoezi 1:1**

1. Kamilisha methali zifuatazo.
(i) Haraka haraka ..........................
(ii) Akili ni .................................
(iii) Kupanda mchongoma.................
(iv) Asiyesikia la mkuu ....................
(v) Haba na haba ...........................
2. Eleza maana ya methali hizi.
(i) Kupotea njia ndiko kujua njia.
(ii) Maji hufuata mkondo.
(iii) La kuvunda halina rubani
(iv) Adui mpende
(v) Mstahimilivu hula mbivu

## Muhtasari wa mada

Katika mada hii, wanafunzi wamejifunza kuhusu:

- Maana ya methali

## Matumizi ya methali

**Mada Kuu 3: Maisha ya watu katika Jamii**

**Somo 1**: Hali za binadamu.

**Malengo**: Baada ya kujifunza funzo hili, utaweza:

- Kutambua watu mbalimbali na kazi zao.
- Kutambua vilema
- Kutambua magonjwa mbalimbali

**Utahitaji vifaa kama**: Muda, daftari, kalamu

**Maagizo**: Tafuta pahali mwafaka kusoma makala haya, utafanya mazoezi na shughuli zote zinaweza kuchukua muda mrefu.Soma maagizo kwa makini kabla ya kufanya zoezi /shughuli husika.

Hali ya binadamu hutokea kwa njia mbalimbali kama kazi zao, maumbile yao na magonjwa yao.

(a) Binadamu hujishughulisha na kazi mbalimbali ili aweze kukidhi maisha yake na familia. Kwa mfano.

| **Kazi** | **Nomino** |
|---|---|
| Udaktari | Daktari (Tibu magonjwa) |
| Ualimu | Mwalimu (Elimisha watu) |
| Uanafunzi | Mwanafunzi (kusoma shuleni) |
| Ukulima | Mkulima (kulima vyakula) |
| Uchungaji | Mchungaji (kuangalia mifugo) |
| Urubani | Rubani (kuendesha) |
| Usonora | Sonora (kuchonga mbao) |
| Ulinzi | Mlinzi (kulinda boma/duka) |

**Shughuli 1:1**

(i) Kusoma kazi mbalimbali za hapo juu

(ii) Andika angalau kazi tano kitabuni mwako.

## **Somo 2:** Upungufu wa mwili

**Malengo**: Baada ya kujifunza funzo hili, utaweza :
- Kutambua watu mbalimbali na upungufu wao wa kimwili.
- Kutambua vilema

**Utahitaji vifaa kama**: Muda, daftari,kalamu

**Utangulizi:**

Je, umewahi kusikia kwamba kuna watu wenye upungufu mwilini?

**Maagizo**: Tafuta pahali mwafaka kusoma makala haya, utafanya mazoezi na shughuli zote zinaweza kuchukua muda mrefu.Soma maagizo kwa makini kabla ya kufanya zoezi /shughuli husika.

## Upungufu wa Mwili

(b) Binadamu pia hubadilika kimaumbile kulingana na upungufu fulani. Kwa mfano;

| NOMINO | UPUNGUFU WA MWILI |
|---|---|
| 1.Kiwete | Mlemavu sana wa mikono na miguu |
| 2.Kibogoyo | Ukosaji wa meno mdomoni |
| 3. Kipofu | Ukosefu wa kuona kitu chochote |
| 4. Kiziwi | Ukosefu wa kusikia sauti |
| 5. Bubu | Ukosefu wa kuongea |
| 6.Macho ya Kengeza | Macho yanayoangalia kiupande |

**Shughuli: 2:1**

(i) Kusoma upungufu wa mwili.

(ii) Kuandika kuhusu upungufu wa mwili.

## **Somo 3:** Magonjwa mbalimbali

**Malengo**: Baada ya kujifunza funzo hili, utaweza :
- Kutambua magonjwa mbalimbali.
- Namna ya kujikinga magonjwa hayo

**Utahitaji vifaa kama**: Muda, daftari,kalamu

**Utangulizi:**

Je, umewahi kugundua kuwa kuna magonjwa mbalimbali duniani?

**Maagizo**: Tafuta pahali mwafaka kusoma makala haya, utafanya mazoezi na shughuli zote zinaweza kuchukua muda mrefu.Soma maagizo kwa makini kabla ya kufanya zoezi /shughuli husika.

## Magonjwa mbalimbali

Binadamu pia hukumbwa na magonjwa mbalimbali duniani kama:

1.Kifaduro (kuhara damu na kutapika)

2.Kifafa (kujiangusha bila kujua)

3. Kaswende (magonjwa ya zinaa)

4. Malale (huambukizwa na mdudu mbung'o)

5. Sarakani (kansa)

6. Upele (kujikunakuna mwilini mwote)

7. Ukimwi (ukosefu wa kinga mwilini)

8. Kuhara (kwendesha)

9. Kutapika (kurudisha chakula mdomoni)

10. Punguani (ukosefu wa akili timamu)

11. Korona (virusi vya korona)

12.Kisukari (ukosefu wa sukari mwilini)

13. Ebola nk

## Magonjwa haya husababishwa na mazingira mbalimbali kama:

-kuumwa na mdudu
-kulala ovyo kingono
- kushika vitu mbalimbali vilivyoshikwa na mtu
-kula vibaya
-kutofanya vizuri kwa mshipa ubongoni
-kukosa vyakula muhimu mwilini

**Njia ya kujikinga na uambukizi wa magonjwa:**

-Tuwe uaminifu kwa wake wetu nyumbani.

-Tuishi kwa mazingira mazuri au safi yasiyokuwa na vichaka.

- Tusikaribie wagonjwa wengine

- Tufuate maagizo ya madaktari kila kunapotokea jambo la magonjwa kama Korona

**Shughuli 3:1**

(i) Taja angalau njia tatu ambazo unaweza kutumia kwa kuwasaidia walemavu.

**Zoezi 1:1**

1. (a)Taja magonjwa mengine na maambukizi yake.

   (b). Toa suluhisho ya kujikinga dhidi ya magonjwa uliotaja hapo juu.

2. Taja kazi mbalimbali za watu zisizotajwa katika hapo juu.

## Muhtasari wa mada

Katika mada hii, wanafunzi wamejifunza kuhusu:

- Kazi mbalimbali
- Upungufu wa mwili
- Magonjwambalimbali
- Namna ya kujikinga dhidi ya magonjwa.

**MWISHO**

NCDC
NATIONAL CURRICULUM
DEVELOPMENT CENTRE

National Curriculum
Development Centre,
P.O. Box 7002,
Kampala.

www.ncdc.go.ug